Hakuna kitu kinachotukuzwa zaidi kwa Allah Mtukufu kuliko dua

Imepokewa kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Hakuna kitu kinachotukuzwa zaidi kwa Allah Mtukufu kuliko dua".

[Ni nzuri (Hasan)] [Imepokelewa na Tirmidhiy, Ibn Majah na Ahmad]

Amebainisha Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa hakuna chochote katika ibada kilicho bora zaidi mbele ya Allah Mtukufu kuliko dua; kwa sababu ndani yake kuna kukiri utajiri wa Allah Mtukufu, na kukiri kushindwa kwa mja na kuhitajia kwake kutoka kwake.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/5509